**Jina:**__________________________________ **Nambari** ______________

**Darasa:** ___________

# MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA MWAKA 2020

**102/2**
**KISWAHILI**
**LUGHA**
**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2 ½**

## KIDATO CHA NNE

for more free exam papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MAAGIZO**

- *Andika* ***jina lako*** *na* ***Nambari yako*** *katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- *Weka* ***sahihi yako*** *na* ***tarehe*** *ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa*
- *Jibu maswali yote.*
- *Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa wazi katika kijitabu hiki cha maswali.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |

***UFAHAMU (ALAMA 15)***

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo**:-

Pengine mwandishi George Orwell alikuwa na maono ya jinsi mataifa mengi ya Kiafrika yangekuwa pindi baada ya kujinyakulia uhuru, alipoandika riwaya ya 'Shamba la wanyama.'

Riwaya hiyo inaakisi hali halisi ya mataifa haya, Kenya ikiwemo, ambapo imejikita katika dhihirisho la jinsi ujenzi wa matabaka ya kitawala, ubinafsi na ukandamizaji wa wananchi, unavyoweza kuzua maasi na hatimaye mapinduzi ya uongozi ulio mamlakani.

Baada ya kuwaambia wanyama kuhusu maono aliyokuwa nayo ya ulimwengu ambao kila mmoja angeishi huru, nguruwe mmoja anayeitwa Old Major, alijenga ari ya wenzake ili kushinikiza ndoto yake, kwa kuandika amri saba ambazo zilihakikisha kuwa rasilimali zote katika shamba hilo zingegawanywa kwa kila mmoja.

Lakini haya yote hayakuzingatiwa muda mfupi baadaye kwani ubinafsi uliokithiri ulichakachua amri hizo na kusambaratisha mfumo wa uongozi katika shamba hilo. Hali hiyo ndiyo tunayoshuhudia kwa sasa, wananchi wanapoandamana katika majimbo mbalimbali kulalamikia 'kodi mpya za maendeleo' zinazoanzishwa na serikali hizo. Huu ndio mkasa wa ubepari, uliojificha katika mfumo kandamizi wa ugatuzi, ambao kwa wazo langu,hatukuwa tumejitayarisha kabisa kuuanzisha.

Tumegatua kila aina ya uovu, umero na wizi. Tulilolisahau ni kuwa 'magavana' hawa tulioamka mapema kuwachagua walikuwa viongozi wale wale waliokuwa wakihudumu katika serikali za hapo awali, na hawakuwa ',miungu wa ukombozi kama walivyotupulizia baragumu zao walipokuwa wakitunadia kila aina ya 'ahadi' wakati wa kampeni.

Kwani ufisadi ndio umekithiri uovu mwingine tulioagatua ni ukabila. Kwa sasa, tofauti zilizopo si za kumchukia Mkikuyu au Mturkana akihiana na Mluo. Kila jamii kwa sasa zinaona wenzao kwa misingi ya kiukoo.

Mathalani, mzozo wa uongozi jimboni Embu unaelezwa 'kuchochewa' na tofauti za uwakilishi kati ya jamii za Waembu na Wambeere. Hapo awali, hatungesikia 'mikataba' kama hii! Huu ni moto uwakapo, kama si safari ya kuzimu tunayoelekea!

Kwani vita vya kikabila havitasikika tena, bali mafarakano yatakayochukua nafasi yake ni 'mizozo ya kiukoo, ambayo katika majimbo yote 47 ni mkasa kama si saratani tuliyojiambukiza.

Ikiwa hatutatahadhari, huenda tukashuhudia maasi ya kiukoo katika nchi ndogo 47' – na kizungumkuti kitakuwa jinsi ya kuyazima, kwani kila koo 'likipigania nafasi yalo.'

for more free exampapers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI**

a) Kwa mujibu wa mwandishi wa makala haya ni mambo yapi yanayoweza kuzua maasi katika nchi ?(alama 3)

b) Eleza mifano miwili ya maovu ambayo yamezungumziwa katika kifungu .(alama 2)

c) “Huu ni moto uwakapo, kama si safari ya kuzimu…..” maneno haya yana maana gani kwa mujibu wa taarifa hii. (alama 3)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

d) Kwa nini mwandishi amefananisha mataifa mengi ya kiafrika baada ya uhuru na shamba la wanyama?(alama 3)

e) Dhihirisha kauli ya mwandishi kuwa ‘tumegatua kila aina ya uovu, umero na wizi.(alama 2)

f) Eleza maana za msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika taarifa (alama2)

(i) Inaakisi…………………………………………………………………………………………

(ii) Mizozo ya kiukoo…………………………………………………………………………

***MUHTASARI (alama 15)***

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Taifa huundwa na watu wanaoishi katika nchi moja na wanaojitambua kisiasa kama watu walio na mwelekeo, maono na hatima sawa. Utaifa hujengwa kwenye misingi ya mapenzi kwa nchi, Utambuzi wa cheo, eneo, hadhi, rangi na hata makabila wanakotoka raia wa taifa moja si chanzo cha kuwatenganisha. Nchi moja huweza kuundwa na watu walio na tofauti chungu nzima zikiwemo tofauti za kikabila, kitabaka na kimawazo. Hata hivyo, watu hao huwa na falsafa na imani sawa kama taifa linaloashiriwa hasa na wimbo wa taifa. Hata hivyo haya yote hayawezi kuwafikia katika kiwango cha kuunda taifa. Uzalendo ndio mhimili mkuu wa utaifa. Uzalendo ni mapenzi aliyo nayo mtu kwa nchi yake. Mapenzi haya humwongoza mtu katika mawazo yake, itikadi yake, matendo yake, matamanio yake na mkabala wake kuhusu nchi na hatima ya nchi yake. Mzalendo hawezi kushiriki katika matendo yanayoweza kuiletea nchi yake maangamizo kwa vyovyote vile. Mzalendo huongozwa na mwenge wa wema.

Mzalendo hawezi kushiriki kwenye shughuli zozote zinazohujumu mshikamano wa kitaifa. Yeye hatawaliwi na ubinafsi wa kutaka kufaidi nafsi yake na ya jamii yake finyu. Matendo yake yote huongozwa na ari ya kuiboresha nchi yake. Anayeipenda nchi yake hujiepusha na ulafi wa kujilimbikizia mali. Yuko radhi kuhasirika mradi taifa lake linufaike. Utaifa ni mche aali unaopaliliwa kwa uzalendo, kuepuka uchu wa nafsi na taasubi hasi zikuwepo za kikabila na ubinafsi. Hali hii inapofikiwa, hatima ya taifa na mustakabali wa raia wake huwa wenye matumaini makubwa.

*(a)* Kwa maneno 40 – 50 dondoa sifa kuu za utaifa.(alama 6, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

for more free exam papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Jibu**

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------ ------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

(b) Ni nini misingi ya kutathmini mzalendo? (maneno 60 - 70) (alama 9, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

for more free exam papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**Jibu**

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------ ------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

**MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) (i) Eleza maana ya sauti za likwidi.(alama 1)

(ii) Tolea mifano miwili ya sauti za likwidi.(alama 1)

(b) Tunga neno lenye muundo ufuatao:

Konsonanti , Kiyeyusho, Irabu Konsonanti Irabu Konsonanti Irabu

(c) Ainisha viambishi katika sentensi hii , kimuundo na kidhamira. (alama 4)

Watamsomesha

for more free exam papers visit: www.freekcsepastpapers.com

(d) Bainisha kiima, kiarifa, kipozi na kitondo katika sentensi ifuatayo. (alama 4)

Jacob alimjengea Halima nyumba nzuri.

(e) Huku ukitolea mifano, eleza matumizi mawili ya kistari kifupi katika uakifishaji.(alama 2)

(f) Tunga sentensi ukitumia vivumishi vinavyoleta maana zifuatazo

(i) kutobagua ( alama 1)

(ii)  kumiliki ( alama 1)

(g) Andika sentensi ifuatayo katika usemi taarifa. ( alama 2)

“ Nitawapa zawadi mwaka ujao.” Mkurugenzi alitwambia.

for more free exam papers visit: www.freekcsepastpapers.com

(h) Nomino hizi ziko katika ngeli gani?

(i) kipepeo ( alama 1)

(ii) maiti (alama 1)

(i) Changanua sentensi hii kwa kutumia kielelezo cha mstari. (alama 2)

Mzee aliyefika hapa atamleta mtoto mdogo leo

(j) Andika neno lenye muundo ufuatao. (alama 2)

(i) Nafsi ya tatu wingi, wakati uliopo, mzizi, kauli tendwa, kiishio

(ii) kiambishi cha wingi, mzizi

(k) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. ( alama 2)

Nomino, kishazi tegemezi, kitenzi nomino

(l) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo. ( alama 2)

Watu wale wote walikuwa wasomi sana.

(m) Tunga sentensi moja ili kuleta maana mbili za neno **paka**.

(n) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maigizo. ( alama 2)

(i) Peter, Kelvin na Musa ndio watapewa vitabu. (Tumia Kiwakilishi nafsi badala ya nomino zilizopigiwa mstari)

(ii)Yusufu alimsomea Rahman hadithi. ( Geuza sentensi hii iwe kwenye kauli ya kutendewa)

(o) Tolea maana nne za sentensi hii. ( alama 4)

Bakari alimpigia Otieno mpira.

(p) Anza sentensi ifuatayo kwa yambiwa. ( alama 1)

Juma alimlimia  Wafula shamba kwa trekta

for more free exam papers visit: www.freekcsepastpapers.com

(q) Fafanua maana za istilahi hizi. ( alama 3)

(i) kishazi tegemezi

(ii) kibadala

(iii) mofimu

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

Fafanua changamoto zozote kumi zinazokumba lugha ya Kiswahili nchini Kenya.

for more free exam papers visit: www.freekcsepastpapers.com